Githaiga Kihara anafanua jambo wakati wa ziara yetu katika shamba la Moo Fodder Supermarket. Nyuma ni shamba la Napier wa Australia waliokomaa (pennisetum purpureum) Bi Kihara katika kitalu cha nacedero (trichantera giganthera) shambani hapo. Picha: KNA

k vine na signal grass (brachiaria brizantha) pamoja na Nacedero (trichanthera gigantea). Ni kutokana na aina hizi za malisho ndipo Kihara amejijengea jina lake ndani na nje ya nchi. "Nilianza mradi huu takriban miaka kumi iliyopita huko Gakindu, Kaunti Ndogo ya Mukuru-rwe-ini, kutokana na mahitaji kwa sababu nilikuwa na mbuzi wa maziwa ambao hawakuwa na chakula cha kutosha. Nilipofanya utafiti, niligundua kwamba naweza kupata chakula bora zaidi na nikaamua kuanzisha," aliamba KNA shambani. Kihara alianza kwa kupanda majani ya signal grass kwa msaada wa kituo cha wakati huo cha Kenya Agricultural Research Institute (sasa KALRO) kilichopo Katumani, Machakos. Jaribio hili moja ndilo lililofungua milango ya kuanzishwa kwa aina nyingine za malisho kama vile Australian Red Napier ambayo sasa imekuwa bidhaa muhimu katika biashara yake. Leo, shamba lake

husafirisha vipandikizi vya red Napier kwa wakulima katika nchi nyingine 12 za Afrika ikiwemo Nigeria, Congo na Sierra Leone. Hata hivyo, mafanikio haya, kwa mujibu wake, hayangeweze kana bila kutumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kama Facebook, WhatsApp, Instagram na TikTok ambapo biashara yake huulikana kwa jina la Moo Fodder Supermarket. "Nilipoanza kuposti bidhaa zangu kwenye ukurasa wangu wa Facebook, watu walianza kuuliza na hivyo ikawa biashara. Hali hii iliendelea hadi nikapata kile ninachoweza kuita mafanikio makubwa nilipopata oda ya vipandikizi milioni moja," anaeleza. Baada ya kufanikiwa kupata wateja wake wa kwanza, Kihara aliendelea kutafuta aina nyingine za malisho na akaanzisha Super Napier ambayo anasema ilifanya vizuri sana.



REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST (REOI) (FIRM CONSULTANCY SERVICE)

KENYA

TRANSMISSION NETWORK IMPROVEMENT PROJECT

Project ID:	P-KE-FA0-022
Project Name:	Transmission Network Improvement Project (KTNIP)
Assignment title:	Annual Environmental and Social Performance Audit (ESPA)
Financing agreement reference:	AfDB and EDCF Loan No. 2000200006058
Tender Name:	Request for Expression of Interest for Consultancy Services for Annual Environmental and Social Performance Audit (ESPA)
Tender No:	KETRACO/PT/032/2025-2026

The Government of Kenya has received financing from the African Development Bank (AfDB) and the Korean Exim Bank (EDCF) towards the cost of the Kenya Transmission Network Improvement Project (KTNIP) and intends to apply part of the proceeds to eligible payments under the contract for Consultancy Services for the Annual Environmental and Social Performance Audit (ESPA).

1. Objective of the Assignment

The objective of this consultancy is to assess the project's compliance with applicable environmental and social (E&S) requirements, including relevant national legislation, AfDB's Integrated Safeguards System (ISS, 2023), and Good International Industry Practice (GIIP). The audit will cover KTNIP components, including more than 270 km of high-voltage transmission lines and associated substations across Western and Coastal Kenya.

2. Scope of Work

The consultant will be required to, among other tasks:

- Review and verify the implementation and effectiveness of E&S instruments and commitments (e.g., ESIA, ESMP, RAP).
- Assess labour and working conditions, including occupational health and safety (OHS) and community health and safety.
- Assess stakeholder engagement, the grievance redress mechanism (GRM), and gender mainstreaming measures.
- Identify gaps and non-compliances and prepare a comprehensive Corrective Action Plan (CAP).
- Prepare and submit audit reports that meet National Environment Management Authority (NEMA) requirements and AfDB standards.

3. Requirements for Consultants

KETRACO now invites eligible consulting firms to indicate their interest in providing these services. Interested consultants shall provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the services.

- Firm profile: Evidence of registration and good standing with NEMA as a firm of experts, with a valid practising licence.
- General experience: At least ten (10) years' experience conducting ESIA's, environmental audits, and RAPs for large-scale infrastructure projects.
- Specific experience: Proven experience in conducting at least two (2No.) E&S performance audits for energy transmission or similar infrastructure projects preferably financed by AfDB or other equivalent DFI.
- Technical capability: Demonstrated experience applying AfDB's Integrated Safeguards System (ISS) and relevant international labour standards.

4. Selection Criteria

Eligibility criteria, the establishment of the short-list, and the selection procedure shall be in accordance with the African Development Bank's "Rules and Procedures for the Use of Consultants" (May 2006 Edition, revised July 2012), which is available on the Bank's website.

Consultants may associate with other firms in the form of a joint venture and/or sub-consultancy to enhance their qualifications.

5. Submission Details

Expressions of interest must be delivered in a written form and clearly marked with the Assignment Title & Tender No. to the address below in person or by mail, or by fax, or by e-mail by **1000 Hours on 23rd June 2026**.

Physical Expressions of Interest to be submitted at Kenya Electricity Transmission Company Limited, Kawi Complex, Block B, South C, Nairobi, Kenya, 2nd floor, Supply Chain Management Office Tender Box by **23rd June 2026 at 10:00AM EAT**. Clearly indicate/mark the submission as "Expression of Interest: for Consultancy Services for Annual Environmental and Social Performance Audit (ESPA) for KTNIP".

Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours [weekdays Monday to Friday 0730hrs to 1630hrs local time excluding public holidays].
rwasa@ketraco.co.ke gmirasi@ketraco.co.ke; cng'enh@ketraco.co.ke; kettenders@ketraco.co.ke

**Attn: Senior Manager; Supply Chain Management
Kenya Electricity Transmission Company Limited (KETRACO)
KAWI Complex, Block B, Popo Lane, off Red Cross Road
P.O. Box 34942-00100, Nairobi, Kenya**

Afueni kwa wakuzaji pamba Yatta wakipokea dawa za kuua wadudu

NA MUOKI CHARLES

Zaidi ya wakulima 1,000 zwa pamba Ndalani na maeneo jirani ya kaunti ndogo ya Yatta, Machakos, wamepatiwa viutilifu na mashine za kisasa za kunyunyizia dawa katika mpango unaoungwa mkono na serikali unaulenga kuongeza uzalishaji wa mazao yanayostahimili ukame katika eneo hilo nusu-kame.

Msaada huo, ulioteklezwa kupitia Mamlaka ya Kilimo na Chakula (AFA), uliwalenga wakulima kutoka makundi ya Ndalani, Kisiiki, Kiwanzani, Nthungululu, Mbembani, Kivungoni na Kakongo. Mpango huo unalenga kupunguza gharama za uzalishaji, kuboresha udhibiti wa wadudu na kuongeza mavuno ya pamba katika eneo ambalo kwa sasa zao hilo limekuwa chanzo

cha uhakika cha mapato kutokana na uwezo wake wa kustahimili hali ngumu ya hewa. Akizungumza wakati wa zoezi la ugawaji, Mkurugenzi wa Umoja wa Wakulima wa Pamba Kitaifa na Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Wakulima wa Pamba cha Ndalani, Francis Kilango, aliwataka viongozi kuweka kipaumbele katika uwekezaji wa kilimo kinachozingatia mabadiliko



Wakulima wa Ndalani katika Kaunti Ndogo ya Yatta wananufaika na dawa za kuulia wadudu wa pamba na mashine za kupulizia kutoka kwa serikali.

ya tabianchi ili kuboresha maisha ya wananchi wa eneo hilo.

“Viongozi, wawe waliochaguliwa au wanaowania nafasi, wanapaswa

kuwasaidia wakulima kukumbatia mazao yanayostahimili ukame kama pamba na alizeti. Mazao haya hufanya vizuri hata katika maeneo yenye

mvua zisizo za uhakika na huwapatia wakulima faida bora,” alisema Kilango. Alibainisha kuwa pamba imekuwa nguzo muhimu ya uchumi kwa maelfu ya kaya katika eneo la Yatta, ikiipatia jamii chanzo cha uhakika cha mapato hata wakati wa ukame wa muda mrefu.

Wakulima wakiongozwa na Daniel Nzioki waliunga mkono mpango huo, wakisema mashine za kunyunyizia dawa zinazotumia jenereta zitaisaidia kuboresha udhibiti wa wadudu, kupunguza gharama za kazi na kuongeza uzalishaji.

Mradi wa Nyumba za bei nafuu wa Kisumu wachochea ukuaji uchumi



Mradi wa Makazi ya bei nafuu wa Upper Kanya kwar (AHP) mjini Kisumu ukiendelea. Ni mojawapo ya miradi mingi ya AHP ambayo serikali inatekeleza kote nchini ili kuboresha upatikanaji wa makazi kwa Wakenya wengi.

NA MABEL KEYA – SHIKUKU NA SALMA OMOLLO (KNA)

KWA TAKWIMU


2.8bn

Ulimwenguni kote, takriban watu 2.8bn wakosa makazi ya kutosha, ardhi salama, na huduma za msingi za maji na mazingira safi

Mgogoro wa makazi duniani ni suala zito, ambapo sehemu kubwa ya watu duniani haina makazi ya kutosha, nafuu, na salama. Makadirio ya Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-Habitat) yanaonyesha kuwa watu bilioni tatu watahitaji makazi bora zaidi kufikia 2030. Sababu kuu za mgogoro huu wa kimataifa ni pamoja na ukuaji wa haraka wa miji unaozidi kasi ya ujenzi wa makazi, ongezeko la idadi ya watu, pamoja na kupanda kwa gharama za ujenzi kutokana na uhaba wa ardhi, nguvu kazi na vifaa vya ujenzi. Mgogoro huu ni mkali zaidi katika maeneo yanayokua kwa kasi mijini na unazidishwa na mabadiliko ya tabianchi, huku mamilioni ya watu wakiishi katika mazingira duni au


kukabiliwa na ukosefu wa makazi kabisa. Takwimu za UN-Habitat zinaonyesha kuwa kufikia mwaka 2030, takriban watu bilioni tatu (3) watahitaji makazi ya kutosha, jambo linaloamaanisha uhitaji wa kujenga vitengo 96,000 vya makazi nafuu kila siku. Duniani kote, takriban watu bilioni 1.12 wakiishi kwenye makazi duni (slums) au makazi yasiyo rasmi. Takriban watu milioni 100 duniani wanakadiriwa kukosa makazi

kabisa. Karibu mtu mmoja kati ya wanne anaishi katika mazingira yanayodhuru afya, usalama na ustawi wake. Mgogoro huu ni mkali zaidi katika maeneo yanayokua haraka kama Afrika na Asia-Pasifiki, ambapo asilimia 62 ya makazi ya mijini barani Afrika na zaidi ya watu milioni 500 katika Asia-Pasifiki hawana upatikanaji wa huduma za msingi za maji. Watu wanaoishi katika makazi duni pia wako katika hatari kubwa ya kukumbwa na joto kali, majanga makubwa ya hali ya hewa na uhaba wa maji. Ukuaji wa haraka wa miji na ongezeko kubwa la watu ni baadhi ya sababu kuu zinazopel- eke kuongezeka kwa makazi yasiyo rasmi. Mambo kama uhaba wa ardhi, upatikanaji mdogo wa mikopo, nguvu kazi, na vifaa vya ujenzi yamefanya makazi kuwa magumu kumudu kwa wengi.



**MINISTRY OF YOUTH AFFAIRS,
CREATIVE ECONOMY AND SPORTS**

REPUBLIC OF KENYA



STATE DEPARTMENT FOR YOUTH AFFAIRS AND CREATIVE ECONOMY
(Office of the Principal Secretary)

NOTICE OF SALE BY PUBLIC AUCTION

REF NO. SDYACE/AUC/01/2025-2026

The State Department for Youth Affairs and Creative Economy (SDYACE) WILL CONDUCT A Public Auction for sale of various boarded items as detailed in the catalogue “as is where is” basis and to be carried out at **Talanta Plaza sixth floor small boardroom wing A (Upper hill) from 11:00am on 29th June, 2026.**

Interested bidders must view and assess the conditions of all the items they intend to buy before the Public Auction date indicated above. All items can be viewed at the locations indicated in the catalogue after contacting the officer in charge for viewing arrangements that viewing will be between 16th to 26th from 9.00am and 3.00pm..

The items on sale among others include: toner cartridges, air conditioners, coat hangers, wooden bookshelves, steel cabinet, clerical tables, broken chairs, portrait frames, water dispenser, paper shredder, microwave, utensils cabinets, sofa set, tv stands, wooden doors, door frames, curtain box, partitioning grills, partitioning boards, grilled doors, broken woods, soundproof boards with frames, carpets, used blankets, and vehicles.


CONDITIONS FOR SALE

- The SDYACE and the appointed auctioneer reserve the right to accept or reject an annul the process at any time prior, without thereby incurring any liability to bidders. In case of annulment, all bidders submitted deposit shall be promptly returned to the bidders.
- Interested bidders are required to pay a refundable deposit of 10% of the reserve price for each lot/item they are interested in. This will be the basis of obtaining the bidding number before the auction date.
- The deposit shall be paid in form of cash at the State Department for Youth Affairs and Creative Economy at Talanta Plaza 2nd Floor Wing B, cash office and then a bid number will be allocated. No person without a bid number will be allowed to participate in the auction.
- The successful bidders deposit will be credited to his bid price so that it forms part of the amount of the bid, and the bidder will be required to pay the bid price less the deposit security.
- Unsuccessful bidder's deposit will be discharged or returned as promptly as possible but not later than seven (7) days after the expiration of the period of Auction.
- The issued MR receipts shall be used to obtain the Bidding Number from procurement office at Talanta Plaza, 2nd floor Wing A.
- Potential bidders may download the catalogue containing details of items for disposal from State Department for Youth Affairs and Creative Economy Website (www.youth.go.ke) free of charge or obtain it from the appointed auctioneer.
- All Sales will be subject to the reserve price.
- All purchased items shall be paid for and collected from respective locations where the items are within 7 days from the date of auction failure to which, the department will charge storage at a rate of kshs. 500 per day until collection. If the items are not collected within 14 days, the items will be forfeited to the department, and the bidder shall forfeit the bid deposit.
- The declared purchaser (highest bidder) **MUST** pay 20% of the purchase price in cash for the lots bided at the fall of the hammer and the balance must be paid in cash within fourteen days from the date of the auction, failure to which the initial deposit will be forfeited and the item offered to the second highest bidder.
- The successful bidders shall pay all costs, applicable duties, and taxes associated with the transfer of the purchased item/Asset i.e, motor vehicle.

Further details on the Public Auction, items viewing and location may be obtained from;
Speedman Commercial Agencies

Nacico Chambers 3rd Floor
Moi Avenue, P.O.BOX 35309-00100 Nairobi
Tel: 020-219318 or 0722822374youth

Head Supply Chain Mngement
Talanta Plaza, 2nd Floor Wing A
P.O.Box 34303-001, NAIROBI.
Email Address: procurement@go.ke



Serikali yachukua kupanua programu ya Vilabu vya 4K kupitia ushirikiano



NA WANGARI NDIRANGU (KNA)

Wizara ya Kilimo na Ustawi wa Mifugo imesisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano ili kupanua mpango wa Klabu za 4K na kuhamasisha vijana zaidi kujihusisha na kilimo. Akizungumza katika hafla ya mafunzo ya kilimo kwa vijana na siku ya shamba iliyoandaliwa na AAK Grow (zamani Chama cha Kemikali za Kilimo cha Kenya), Mkuu wa Kitengo cha Vijana katika Kilimo, Charles Lusweti, alibainisha kuwa mpango wa 4K unasaidia kukabiliana na changamoto ya wakulima kuzeeka kwa kuwaingiza wanafunzi katika kilimo wakiwa bado wachanga. Lusweti alisema Klabu za 4K zilizoboreshwa na kuanzishwa upya mwaka 2021 sasa zinafanya kazi katika kaunti zote 47, zikiwa na takriban klabu 2,700 zilizosajiliwa na zaidi ya wanafunzi 300,000 wanaoshiriki.

Alisema mpango huo unawawezesha wanafunzi kujifunza teknolojia za kisasa za kilimo, zikiwemo ndege droni, zana za kidi-jitali na fursa za kilimo-bi-ashara, jambo linalofanya sekta hiyo kuvutia zaidi kwa vijana.

“Klabu mpya ya 4K si kilimo tu. Wanafunzi wanatambulishwa kwa teknolojia, ubunifu na fursa katika mnyororo mzima wa thamani wa

kilimo,” alisema. Lusweti aliwahimiza serikali za kaunti, shule na wadau wa sekta binafsi kuendelea kuunga mkono mpango huo, akisema ushirikiano ni muhimu ili kufikia shule zaidi na kuimarisha usalama wa chakula, lishe na ajira kwa vijana.

Pia alitaja mafanikio ya miradi ya kilimo shuleni katika Kajiado na Embu, ambapo uzalishaji wa kilimo unasaidia programu za chakula shuleni.

Stella Simiyu, Mkurugenzi Mtendaji wa CropLife Africa Middle East, ambayo imeshirikiana na serikali kuunga mkono mipango ya Klabu za 4K, alisifu juhudi za Kenya za kuwashirikisha vijana katika kilimo, akisema uwekezaji wa nchi katika elimu ya kilimo ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula wa baadaye.

Simiyu alisema Kenya ni miongoni mwa nchi tatu zinazotekeleza Mfumo wa Usimamizi Endelevu wa Viuatilifu vya Kilimo, mpango wa miaka mitano unaolenga kuendeleza mbinu endelevu za kilimo,

Kenya ni miongoni mwa nchi tatu zinazotekeleza Mwongozo Endelevu wa Usimamizi wa Dawa za Wadudu

pamoja na Morocco na Misri.

Alisema mpango huo unalenga kuzalisha chakula zaidi kwa rasili-mali chache, kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia za kilimo na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa mifumo ya uzalishaji wa chakula.

Simiyu alibainisha kuwa kuwawezesha vijana kwa maarifa ya kilimo na teknolojia za kisasa kama droni kutasaidia kubadilisha sekta hiyo na kuleta mabadiliko ya kitabia katika jamii.

“Ikiwa unataka kujua imeshirikiana na sekta, angalia vijana,” alisema, akiongeza kuwa watoto wanaweza kueneza kwa ufanisi ujumbe kuhusu mbinu salama za kilimo ndani ya familia na jamii zao.

Alitoa wito mpango unaotekelezwa Kenya kupanuliwa nchini kote na kuigwa katika mataifa mengine ya Afrika, huku akihimiza ushirikiano zaidi kati ya taasisi za serikali, shule, familia, jamii na washirika wa maendeleo. Simiyu alisisitiza kuwa kilimo hakipaswi kuachwa kwa Wizara ya Kilimo pekee, akisema wadau wote wana jukumu la kulea kizazi kijacho cha wakulima.

“Ninataka kuzipa changamoto jamii kuwekeza zaidi katika mipango ya kilimo inayolenga vijana, ukizingatia kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi

1. Charles Lusweti, Mkuu wa Kitengo cha Vijana katika Kilimo ndani ya Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo ya Kenya pamoja na wanafunzi wa klabu ya 4K katika Chuo Kikuu cha Egerton

2. Maeneo ya maonyesho ambapo

wanachama wa klabu ya 4k wanaonyesha baadhi ya mazao wanayolima ndani ya Chuo Kikuu cha Egerton

3. Mkurugenzi Mtendaji wa AAK Grow Joel Mutai akizungumzia ushirikiano na serikali katika kukuza klabu ya 4K

wa Kenya na kichocheo muhimu cha ukuaji wa baadaye,” alisema Simiyu. Naibu Chansela wa Chuo Kikuu cha Egerton, Prof. Isaac Ongubo Kibwage, alisema chuo hicho kinahost mpango wa Klabu za 4K ili kukuza hamasa ya vijana katika kilimo na kuimarisha usalama wa chakula wa baadaye.



REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL GOVERNMENT AFFIRMATIVE ACTION FUND

EMPOWERING FOR SELF-RELIANCE



Website : www.ngaaf.go.ke
Email: ceongaaf@gmail.com

The National Government Affirmative Action Fund NAIROBI COUNTY invites sealed bids from interested and eligible suppliers to tender for **SUPPLY AND DELIVERY OF SANITARY TOWELS TO PUBLIC PRIMARY AND JUNIOR SECONDARY SCHOOLS BY LOCAL MANUFACTURERS AND AGPO CATEGORIES (YOUTH, WOMEN AND PEOPLE WITH DISABILITY-PWD)**, as per the below lots;

LOT	COUNTY	TOTAL NO. OF PACKETS (8 Pieces per Packet)	RESERVED
Lot 1	Embakasi south	18,651	Manufacturers
	Embakasi east	19,567	
	Embakasi central	32,094	
	Embakasi west	33,237	
	Langata	12,039	
	Njiru	19,638	
Total No. of Packets (Lot 1)		159,513	
Lot 2	Starehe	21,333	AGPO
	Westlands	31,377	
	Kamukunji	17,913	
	Kasarani	10,497	
Total No. of Packets (Lot 2)		81,120	
Lot 3	Makadara	27,948	AGPO
	Roysambu	28,113	
	Mathare	19,311	
Total No. of Packets (Lot 3)		75,372	
Lot 4	Ruaraka	12,867	AGPO
	Dagoretti south	28,623	
	Dagoretti north	22,662	
	Kibra	16,515	
Total No. of Packets (Lot 4)		80,667	

Eligible bidders may download a complete set of tender documents including the evaluation criteria, from the PPIP portal: www.tenders.go.ke (<http://www.tenders.go.ke>) or from NGAAF website www.ngaaf.go.ke, using the Tender Reference Number, **free of charge**.

Completed Tender documents clearly marked with the Tender No. and Lot No, should be deposited in the Tender Box located at **Nyayo House, 8th Floor Room 14**.

Addressed to: **The County Coordinator; Nairobi County, National Government Affirmative Action Fund, P.O. Box 983 - 00100, Nairobi -Kenya**

Tenders must be received on or before **Monday 29th June 2026 at 10:00AM Local Time**. Tenders will be opened immediately afterward in the presence of bidders or their representatives who choose to attend at Nyayo house, 8th floor, room 14 County Coordinator's office as will be led by the officer in charge. Late applications will not be accepted.

THE COUNTY CO-ORDINATOR, NAIROBI COUNTY, NATIONAL GOVERNMENT AFFIRMATIVE ACTION FUND

Hifadhi ya Nishati ya Kijani ya Olkaria ya KenGen sasa eneo linalodhibitiwa na forodha

NA ERASTUS GICHOHI
(KNA)

Kampuni ya Kenya Electricity Generating Company (KenGen) imefikia hatua muhimu ya udhibiti kwa Hifadhi yake ya Nishati Safi iliyopo Olkaria, Naivasha, baada ya kutangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali kuwa Eneo Linalodhibitiwa na Forodha. Hatua hiyo inafungua fursa za motisha za kodi na forodha chini ya mfumo wa Kanda Maalum za Kiuchumi (SEZ), na hivyo kuimarisha hadhi ya eneo hilo kama kitovu cha maendeleo ya viwanda vinavyotumia nishati safi. Hadhi hiyo ilitolewa kwa kampuni ya KenGen Energy Services (SEZ) Limited kupitia tangazo la Kamishna wa Forodha na Udhibiti wa Mipaka, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa KenGen, Mhandisi Peter Njenga, mpango huo ni sehemu ya juhudi pana za kampuni hiyo za kukidhi ongezeko la mahitaji ya nishati huku ikipunguza kiwango cha utoaji wa hewa ukaa nchini Kenya, sambamba na lengo la serikali la kuhamia matumizi ya asilimia 100 ya nishati safi ifikapo mwaka 2030. Mhandisi Njenga alisema kutambuliwa kwa Hifadhi ya Nishati Safi kama Eneo Linalodhibitiwa na Forodha kunafungua kikamilifu fursa za uwekezaji wa SEZ huko Olkaria, na kuimarisha nafasi ya eneo hilo kama kitovu cha viwanda barani Afrika vinavyotumia nishati ya jotoardhi.



Mojawapo ya kiwanda cha kuzalisha umeme wa jotoardhi katika eneo la Olkaria mjini Naivasha ambapo Kampuni ya Kuzalisha Umeme ya Kenya (KenGen) imeanzisha hifadhi ya nishati ya kijani ya zaidi ya ekari 8,000 ambapo wawekezaji watafikia ushuru wa umeme wa moja kwa moja na wa chini, ushuru wa forodha uliopunguzwa na unafuu wa kodi. PICHA: ERASTUS GICHOHI

SEZ ya Olkaria inatarajiwa kuvutia viwanda mbalimbali kuanzia usindikaji wa mazao ya kilimo, utengenezaji wa nguo, uzalishaji wa teknolojia ya usafiri wa umeme hadi vituo vya kuhifadhi na kuchakata data. Hatua hiyo inawezesha utekelezaji wa motisha za kodi zinazotolewa kwa wawekezaji chini ya Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi ya mwaka 2015 na kuigeza hifadhi hiyo kuwa eneo linalofanya kazi kikamilifu kwa shughuli za viwanda na uwekezaji. Kutambuliwa kwa eneo hilo kama Eneo Linalodhibitiwa na Forodha kutafanya hifadhi hiyo kufaidika na taratibu maalum za forodha, maeneo yanayodhibitiwa ya kuingia na kutoka pamoja na mifumo ya udhibiti wa

uzingatiji wa sheria kwa bidhaa zote zinazolingia, kusafirisha ndani au kutoka katika eneo hilo. Hatua hiyo itahakikisha kuwa vituo vya forodha, malango maalum, mifumo ya kuhifadhi bidhaa chini ya dhamana na mifumo ya uzingatiaji wa sheria vinakuwa sehemu zinazotambulika kisheria katika shughuli za hifadhi hiyo. Hadhi hiyo pia inafungua manufaa halisi ya SEZ, yakiwemo kurahisishwa kwa taratibu za uagizaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi, ufanisi katika ushuru na kodi, kuharakishwa kwa utoaji wa mizigo bandarini na kurahisishwa kwa usimamizi wa kisheria, hali ambayo itaondoa sintofahamu za udhibiti zinazojitokeza kabla ya maeneo ya SEZ

kuanza kufanya kazi kikamilifu. KenGen pia imefikia mipango ya kuomba leseni ya kusafirisha na kusambaza umeme moja kwa moja kwa viwanda vitakavyoanzisha shughuli zake katika Hifadhi ya Nishati Safi, ikitegemea Kanuni za Nishati (Soko la Umeme, Ugavi wa Jumla na Ufikiaji Huria) za

KWA TAKWIMU

1,500

KenGen imejitolea kuongeza MW 1,500 za ziada za nishati ya kijani kwenye gridi ya taifa ifikapo 2034 kwa kukusanya zaidi ya Sh.400 bilioni kupitia uwekezaji wa umma na binafsi.

mwaka 2026 ambazo zimeruhusu kampuni zinazozalisha umeme kuuza umeme moja kwa moja kwa watumiaji wakubwa. Mpango huo unaweza kuwapa wawekezaji wa viwanda viwango vya bei ya umeme vilivyo chini ya viwango vya kawaida vya rejareja, jambo litakaloongeza ushindani wa hifadhi hiyo. Hifadhi hiyo ya nishati safi iko ndani ya maeneo ya jotoardhi ya Olkaria, Naivasha, ambayo ni makazi ya mojawapo ya hazina kubwa zaidi za jotoardhi duniani, na kuwapa wawekezaji nishati safi ya asilimia 100 isiyokatizwa, manufaa yote ya SEZ na upatikanaji wa moja kwa moja wa mvuke wa jotoardhi. SEZ hiyo ina ukubwa wa zaidi ya ekari 8,000 na imeundwa kuwa kichocheo muhimu cha uwekezaji wa viwanda, utengenezaji wa bidhaa kwa kutumia nishati safi na uzalishaji unaozunguza masoko ya nje, huku eneo lake la kimkakati kando ya njia kuu za usafiri, ikiwemo Reli ya Kisasa (SGR), likiawezesha wawekezaji kufikia kwa urahisi masoko ya ndani na ya kikanda. KenGen inaendeleza hifadhi hiyo kwa awamu nne zitakazokamilika ifikapo mwaka 2045, na kuibadilisha Olkaria kutoka eneo la uzalishaji wa nishati pekee kuwa jiji kamili la viwanda vya kijani. Hifadhi hiyo tayari imepokea wawekezaji watano kutoka sekta muhimu za kimkakati, zikiwemo vituo vya data, uzalishaji wa mbolea ya kijani, teknolojia ya usafiri wa umeme, utengenezaji wa bidhaa za chuma, usafirishaji na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Miongoni mwa waliokwisha kujitolea kuwekeza ni Synergetic Development Group, ambayo imesaini makubaliano ya kuanzisha kituo jumuiishi cha usafirishaji wa bidhaa za chuma na kiwanda cha kutengeneza bidhaa za chuma katika hifadhi hiyo, kwa kutumia megawati 18 za umeme wa jotoardhi, ekari 10 za ardhi na mita za ujazo 360 za maji kila mwaka.

Makundi ya Kenya, Denmark yatia saini mkataba wa kibiashara

NA ANITA KARIUKI (KNA)

Muungano wa Sekta Binafsi Kenya (KEPSA) na Chama cha Biashara cha Denmark (DCC) zimetia saini makubaliano ya kimkakati ya ushirikiano yanayolenga kuimarisha biashara, uwekezaji na ushirikiano wa kibiashara kati ya Kenya, Afrika Mashariki na Denmark. Makubaliano hayo, yaliyotia saini katika makao makuu ya KEPSA jijini Nairobi, yanalenga kuboresha upatikanaji wa kampuni za Denmark katika masoko ya Kenya na Afrika Mashariki kupitia majadiliano ya sera, uhusiano wa kibiashara, urahisishaji wa biashara na upatikanaji wa taarifa za masoko. Ushirikiano huo pia utazingatia ziara za kibiashara, mipango ya kubadilishana uzoefu, ujenzi wa

minyororo endelevu ya thamani, ushirikiano wa ndani pamoja na uundaji wa nafasi za ajira. Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini wa makubaliano hayo, Afisa Mkuu Mtendaji wa KEPSA, Carole Kariuki, alisema kuwa makubaliano hayo yanathibitisha nafasi ya Kenya inayozidi kuimarika kama kitovu kinachopendelewa kwa uwekezaji na lango la kuingia katika eneo la Afrika Mashariki. “Ushirikiano wa KEPSA na Chama cha Biashara cha Denmark (DCC) ni uthibitisho thabiti wa nafasi ya Kenya kama lango la Afrika Mashariki na mahali pa kuaminika kwa uwekezaji na biashara,” alisema Kariuki. Alibainisha kuwa kwa kuunganisha biashara za Denmark na mfumo wa sekta binafsi wa Kenya, ushirikiano huo utaimarisha fursa



Sarah Jordan Torp (aliyeketi kushoto) kutoka Chama cha Biashara cha Denmark na Dkt. Jackson Koimburi, Mkuu wa KEPSA Consult na Mratibu Mkuu wa Uchumi na Mabadiliko ya Tabianchi (aliyeketi kulia), wakisaini makubaliano ya ushirikiano kwa niaba ya Chama cha Biashara cha Denmark (DCC) na Muungano wa Sekta Binafsi ya Kenya (KEPSA), mtawalia.

za biashara, uwekezaji endelevu, ubunifu, upanuzi wa masoko na uundaji wa ajira katika eneo lote. KEPSA inawakilisha zaidi ya biashara milioni mbili nchini Kenya kupitia mtandao wa zaidi ya vyama 80 vya sekta na biashara, jambo linaloifanya kuwa mojawapo ya mashirika makubwa zaidi ya sekta binafsi nchini. Makamu wa Rais wa Chama cha Biashara cha Denmark, Jakob Ellemann-Jensen, alieleza

Kenya kuwa mojawapo ya masoko yenye kuvutia zaidi kwa ukuaji barani Afrika, hasa katika nyanja za nishati jadidifu, teknolojia ya kidijitali, sayansi za maisha na usafirishaji wa bidhaa. “Kwa sasa, Kenya ni mojawapo ya masoko yenye kuvutia zaidi kwa ukuaji barani Afrika. Kupitia ushirikiano na KEPSA, kampuni za Denmark zitapata jukwaa imara la ndani na fursa ya kufikia mfumo uliopo wa biashara katika Afrika Mashariki,” alisema.

Ellemann-Jensen aliongeza kuwa ushirikiano huo utasaidia kuimarisha uhusiano kati ya kampuni za Denmark na masoko ya Afrika Mashariki huku ukihamasisha uwekezaji wa muda mrefu na ukuaji endelevu wa uchumi. “Tunaona fursa kubwa katika kujenga madaraja imara zaidi kati ya kampuni za Denmark na masoko ya Afrika Mashariki. Hili si suala la biashara pekee, bali pia la kujenga ushirikiano wa muda mrefu, uwekezaji na ukuaji wa pamoja,” alisema. Ushirikiano huo unaendana na ajenda pana ya Denmark ya maendeleo ya kimataifa, inayolenga kuunganisha maendeleo ya kiuchumi, upanuzi wa masoko na uundaji wa ajira. Kupitia Mpango wa Ushirikiano wa Denmark na Nchi za Kiarabu (DAPP), Chama cha Biashara cha Denmark kwa kushirikiana na PlanBørnefondten, katika miaka ya hivi karibuni kimekuwa kikisaidia ujasiriamali, mifumo ya kuanzisha biashara mpya na mipango ya ajira kwa vijana katika eneo la Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini.


Kenya yaangazia ripoti za marufuku ya ajira kwa wajakazi nchini Kuwait

NA JULIUS NDEGWA (PCO)

Serikali ya Kenya imewahakikishia wanaotafuta ajira na wadau wa uhamiaji wa kazi kufuatia ripoti zilizoenea zikidai kuwa Kuwait imeweka marufuku mpya ya kuajiri wafanyakazi wa nyumbani kutoka Kenya. Katika taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Kenya nchini Kuwait tarehe 10 Juni, serikali ilifanua kuwa Kenya haijapigwa marufuku upya kutuma wafanyakazi wa nyumbani kwenda Kuwait ulisitishwa kwa hiari na Kenya karibu muongo mmoja uliopita na bado msimamo huo unaendelea kutumika. Ufafanuzi huo umefuatia ripoti kutoka vyombo vya habari vya kikanda na kimataifa kwamba Kuwait imezuia ujiri wa wafanyakazi wa nyumbani kutoka nchi 10 zilizodhinishwa huku ikiwatenga wengine 27, zikiwemo Kenya, chini ya kanuni mpya zilizorekebisha zinazosimamia sekta ya ajira ya wafanyakazi wa nyumbani. Kwa mujibu wa Ubalozi wa Kenya, mawasiliano ya hivi karibuni kutoka kwa mamlaka za Kuwait yanaakisi tu hali iliyokuwepo kwa muda mrefu na hayapaswi kutafiriwa kama sera mpya inayolenga Kenya au wafanyakazi wa Kenya. “Kenya haijapigwa marufuku upya kutuma wafanyakazi wa nyumbani Kuwait. Serikali ya Kenya ilisitisha kwa hiari uhamiaji wa wafanyakazi wa nyumbani kwenda Kuwait takribani miaka kumi iliyopita, na msimamo huo bado unaendelea,” ubalozi ulisema. Ufafanuzi huo umejiri baada ya ripoti kadhaa za vyombo vya habari kuonyesha waraka uliotolewa na Wizara ya Mambo

ya Ndani ya Kuwait ukipunguza ujiri wa wafanyakazi wa nyumbani kwa nchi zilizodhinishwa kama Afrika Kusini, Ethiopia, Filipino, India, Nepal, Sri Lanka na Vietnam, huku Kenya na nchi nyingine kadhaa za Afrika zikizuiwa. Ubalozi ulisitiza kuwa vuzuizi hivyo vinahusu tu kundi la wafanyakazi wa nyumbani na haviathiri sekta nyingine ambapo Wakenya bado wanaendelea kupata ajira nchini Kuwait. “Makundi mengine yote ya wafanyakazi wa Kenya bado yanastahili kutafuta fursa za ajira nchini Kuwait kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazotumika za nchi zote mbili,” taarifa hiyo ilibainisha. Kenya na Kuwait kwa sasa zinafanya mazungumzo yanayolenga kuunda mfumo wa pande mbili wa kazi utakaoweka taratibu, ulinzi na mifumo ya kusimamia ushirikiano wa baadaye katika sekta ya ajira ya wafanyakazi wa nyumbani. Uhamiaji wa kazi umekuwa nguzo muhimu ya mkakati wa ajira wa Kenya, huku maelfu ya vijana wakitafuta fursa nje ya nchi, hasa katika nchi za Ghuba. Kuwait bado ni mojawapo ya maeneo wanayokwenda wafanyakazi wa Kenya, hasa katika sekta za afya, ukarimu, ujenzi na kazi za kiufundi. Ubalozi ulibainisha kuwa wafanyakazi wa Kenya wanaendelea kuwa na sifa nzuri nchini Kuwait kutokana na weledi wao, ujuzi na maadili ya kazi, hali inayochangia pakubwa katika sekta mbalimbali za uchumi wa nchi hiyo. Maendeleo haya yanajiri wakati ambapo Kuwait inaendelea na mageuzi mapana ya soko lake la ajira. Hatua mpya zilizochukuliwa na mamlaka za Kuwait ni pamoja na usimamizi mkali zaidi wa ujiri wa wafanyakazi wa nyumbani, matumizi ya mifumo ya kidijitali katika huduma za

visa na udhamini, pamoja na kanuni zilizorekebisha zinazosimamia ajira ya wafanyakazi wa nyumbani na madereva. Wataalamu wa masuala ya kazi wanasema ufafanuzi huu ni muhimu kwa kuwa taarifa kuhusu marufuku mpya zilikuwa zimesababisha wasiwasi kwa wanaotarajia kwenda kufanya kazi nje ya nchi na mashirika ya ujiri nchini Kenya. Serikali katika miaka ya hivi karibuni imeongeza juhudi za kukuza uhamiaji salama na uliodhibitiwa wa kazi, huku ikipambana na mashirika yasiyo rasmi ya ujiri yanayotuhumiwa kuwanyonya wanaotafuta ajira. Katibu Mkuu wa Idara ya Kazi na Maendeleo ya Ujuzi, Shadrack Mwadime, amewahi kusema kuwa serikali imejikita katika kuimarisha usimamizi wa mashirika binafsi ya ujiri ili kulinda Wakenya wanaotafuta ajira nje ya nchi. Ameerza pia umuhimu wa mifumo ya uwazi na iliyopangwa ya uhamiaji wa wafanyakazi kama sehemu ya ajenda pana ya ajira nchini. Mwadime pia amesema kuwa ajira za nje ya nchi ni sehemu muhimu ya mkakati wa taifa wa kutengeneza ajira, hasa kwa idadi kubwa ya vijana. Akizungumza katika mikutano ya kimataifa ya kazi, amesisitiza kuwa serikali inaendelea kuchukua hatua za makusudi kupanua ajira zenye hadhi bora ndani na nje ya nchi. Ubalozi pia umebainisha kuwa Kuwait mara kwa mara hupitia upya kanuni zake za kazi ili kuboresha usimamizi, kurahisisha taratibu za ujiri na kuimarisha ulinzi kwa wafanyakazi na waajiri. Imehakikishia umma kuwa uhusiano wa uhamiaji wa kazi kati ya Kenya na Kuwait bado uko imara licha ya vuzuizi vya sasa vinavyoathiri wafanyakazi wa nyumbani.



Multimedia University of Kenya

P.O. BOX 15653 -00503, NAIROBI
Tel. +254 20 2071391, Email: vc@mmu.ac.ke Website: www.mmu.ac.ke

TENDER NOTICE


Multimedia University of Kenya invites sealed bids from eligible bidders for the following tenders:

Tender No:	Description of Tender	Tender Security (Ksh)	Eligibility	Closing Date & Time	Pre-Bid Meeting/ Site Visit
MMU/OT/LIB/07/2025-2026	PROPOSED PARTIAL COMPLETION OF MULTIMEDIA UNIVERSITY OF KENYA LIBRARY - (Electrical Works and structured cabling works) subcontract - Retender	600,000	Open	30th June 2026 at 11.00am	Pre-Bid meeting on 23/06/2026 at 10:00am at the New Library Building

Tender documents with detailed information and instructions may be viewed and downloaded from the University's website: www.mmu.ac.ke and the Public Procurement Information portal, www.tenders.go.ke free of charge. Bidders who choose to download the tender documents must forward their company's particulars to procurement@mmu.ac.ke for recording and further addenda/clarifications if any.

Vice Chancellor
Multimedia University of Kenya

Riding on Technology, Inspiring Innovation



TECHNICAL UNIVERSITY OF MOMBASA

P.O. BOX 90420-80100 Mombasa, KENYA
TEL: (+254) 0208095365 / (+254) 0208095368 (+254) 020 8095371/0733 955377
Email: procurement@tum.ac.ke

TENDER NOTICE

Technical University of Mombasa invites sealed tenders from interested and eligible bidders for:

No.	Tender Reference No.	Tender Description	Eligibility
1.	TUM/T/12/2026-2027	PROVISION OF MEDICAL INSURANCE COVER	Open

The tender documents may be obtained by interested tenderer from Technical University of Mombasa website: www.tum.ac.ke or PPIP portal <http://tenders.go.ke> free of charge. Bidders are encouraged to download tender documents to minimize physical visit to TUM Offices.

The **Original plus One Copy** of the complete tender document should be enclosed in plain sealed envelope clearly marked with the tender name and reference numbers and be deposited in Tender box A located at the Administration Block Ground Floor area next to the reception desk on or before **Tuesday 23rd June 2026 at 10.00 a.m. EAT** and addressed to:

THE VICE CHANCELLOR
TECHNICAL UNIVERSITY OF MOMBASA
P.O. BOX 90420-80100 MOMBASA, KENYA

Bids will be opened immediately thereafter at the University Conference Room.

TUM is ISO 9001:2015 Certified

A Technical University of Global Excellence in Advancing Knowledge Science and Technology

Wauzaji wahimizwa kujiunga na vyama vya ushirika kupata usaidizi

NA DAVID NDURO (KNA)

Mamlaka ya Biashara Ndogo na Kati (MSEA) imewahimiza wafanyabiashara wadogo katika Kaunti ya Isiolo kujipanga katika vyama vya ushirika na mashirika ya kibishara ili kuongeza nafasi zao za kupata ruzuku za serikali, mikopo, na programu nyingine za maendeleo ya biashara. Akizungumza wakati wa maonesho ya biashara katika Mji wa Isiolo, Afisa Mkuu Mtendaji wa MSEA, Henry Rithaa, alisema hatua hiyo inaunga mkono mpango mpana wa serikali wa mageuzi ya kiuchumi unaolenga kuwawezesha wafanyabiashara wadogo, wa kati na wa ukubwa mdogo (MSMEs) nchini kote. Bwana Rithaa alisema kuwa

vikundi vilivyoandaliwa rasmi vina uwezekano mkubwa wa kunufaika na mifumo iliyoratibiwa ya msaada, upatikanaji bora wa rasilimali, na hatua zilizopangwa za kuimarisha ukuaji wa biashara na ushindani. Alisisitiza kuwa vyama vya ushirika na mashirika ni muhimu katika kusaidia biashara ndogo kukabiliana na changamoto za pamoja kama vile upatikanaji mdogo wa masoko, ukosefu wa fedha za kutosha, na ukosefu wa ujuzi au uwezo. “Kupitia mipango ya mafunzo, ushirikiano wa wadau, na msaada wa kitaasisi, MSEA inalenga kuanzisha mitandao thabiti ya kibishara inayoweza kuchochea ubunifu, kuzalisha ajira, na kuendeleza maendeleo jumuishi ya kiuchumi,” alisema Rithaa.



Afisa Mkuu Mtendaji wa MSEA Henry Rithaa (wa 2 kutoka kushoto) na Naibu Gavana wa Isiolo Dkt. James Lowasa (wa 4 kutoka kushoto) walipokuwa wakitembelea maonyesho ya biashara wakati wa maonyesho ya biashara katika Mji wa Isiolo kwa hisani ya MSEA na serikali ya Kaunti ya Isiolo..

Alibainisha kuwa sekta kama uzalishaji na uuzaji wa maziwa ya ngamia, ufugaji wa kuku na kilimo cha mboga na matunda, biashara ya mifugo, usindikaji wa ngozi, pamoja na sanaa na ufundi zinaweza kunufaika kwa

kiasi kikubwa na mpango huo. Bwana Rithaa aliwahimiza wazalishaji wa maziwa ya ngamia kuzingatia kuongeza thamani ya bidhaa zao ili kuongeza faida, akibainisha kuwa mipango ya ufadhili ya serikali inaweza kuwasaidia kununua

mashine muhimu na kuanzisha viwanda vya usindikaji. Alitaja machinjio ya kisasa ya Isiolo yanayotarajiwa kama fursa kubwa kwa wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo, huku akiwashauri wazalishaji wa ndani kujiweka tayari kukidhi ongezeko linalotarajiwa la mahitaji ya mifugo mara baada ya kituo hicho kuanza kufanya kazi. Naibu Gavana wa Isiolo, Dkt. James Lowasa, alibainisha kuwa kukamilika kwa Kituo cha Kukusanyia Bidhaa cha Isiolo pamoja na machinjio ya kisasa kutachochea shughuli za kibishara na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi ya kaunti. Dkt. Lowasa pia aliwaomba wawekezaji kufikiria kuanzisha viwanda vya kuchuna ngozi ili kuunga mkono machinjio na kuongeza thamani ndani ya sekta ya mifugo. Kamishna wa Kaunti ya Isiolo, Chaunga Mwachaunga, aliwahimiza wafanyabiashara kutumia kikamilifu programu za serikali zilizoundwa kukuza biashara na kuboresha maisha.

Jitihada za kuokoa familia za mitaani zapunguza idadi ya wahusika maradufu

NA ERASTUS GICHOHI (KNA)

